**P1 – Y2 – KISWAHILI - LUGHA**
**MTIHANI WA MWIGO – PP1**
**MACHI, 2018**
**MUDA: SAA 2½**

**JINA:………………………………………………..**

**NAMBARI YA USAJILI :……………………………**

**UKUMBI: ……………………………………………**

**Maagizo:**

1) Andika Jina lako, Nambari ya usajili na Ukumbi katika nafasi ulizoachiwa.
2) Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi hii.

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI**

| SEHEMU | SWALI | UPEO | TUZO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | JUMLA | | |

## SEHEMU YA 'A' - INSHA (Alama 20)

***"Chagua Mojawapo ya Insha na Uandike maneno yasipungua 450"***

1. Wakenya hawawezi kuafikia umoja wa kitaifa iwapo wataendelea kutumia lugha zao za kienyeji. " Jadili"
2. Wewe kama mwanafunzi umepata nafasi ya kumhoji Mkurugenzi wa Habari nchini kuhusu umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Andika mahojiano hayo.
3. Atangaye sana na jua hujua.
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:
   "……………………. Nilishusha pumzi, nikashukuru. Masaibu yangu yalikuwa yamefika kikomo na maisha ya siku zijazo yalijaa matumaini."

---

## SEHEMU YA 'B' - UFAHAMU(Alama 20)

5. **UFAHAMU**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu mswali yafuatayo;

Mafuta yanayopatikana kwenye fukwe za bahari, moshi wa magari, takataka na bidhaa nyinginezo zinazotupwa hapa na pale ni vichafuzi vya mazingira. Vichafuzi huathiri afya zetu na kuathiri wanyama pamoja na mimea. Wanadamu wanyachafua mazingira yao kwa kila aina ya bidhaa mbaya zakikemikali

zinazotoka viwandani au kwenye viwanda vya kawi au nguvu. Bidhaa hizo ni matokeo ya maisha ya siku hizi anayosihi binadamu.

Licha ya ukweli huu, ni muhimu kujua kuwa uchafuzi wa mazingira haukuanza leo. Miaka na miaka iliyopita, viwanda vimekuwa vikitoa mawingu makubwa ya moshi wenye sumu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira umeongezeka maradufu kutokana na kuongezeka kwa viwanda. Uchafuzi umesambaa ardhini, kwenye anga na majini. Msambao huu unapatikana katika pembe zote za ulimwengu wetu. Je, kuna aina zipi za uchafuzi?

Kwanza kuna uchafuzi wa halianga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulikana kama ozoni. Tabaka hili huwa ni ama ya gesi ya oksijeni na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha saratani ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira unaelekea kuliathiri tabaka hili. Vilevile baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika friji au jokofu au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huu haribu ukanda huo.

Aina nyingine ya uchafuzi ni ile tunayoweza kuuita uchafuzi wa kiajali. Huu ni uchafuzi ambao hutokea kama ajali, yaani binadamu hatendi kimakusudi. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. Mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingira yenyewe.Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari.

Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hili huweza kuiua mimea. kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama wa pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hutoa moshi uliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa unaopatikana katika mazingira mengine yetu ni utupwaji ovyo wa takataka. Fauka ya hayo, watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya kupenyeza kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila ya kujali wala kubali. Takataka hizi ni kama makopo, mifuko ya plastiki,mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto. Aidha, takataka hizi hufanva mazingira yetu yaonekane machafu.

Sote tunajukumu kubwa la kuchangia kupunguza uchafuzi wa kimazingira ya kwanza ni kuelimishana na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu. Tunapaswa kutia takataka zetu katika vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuziteketeza. Njia nyingine ni kuhakikisha kuwa tunatunza vitu kama mifuko, chupa na kadhalika ambavyo huweza kuunda upya na kutumiwa tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni. kumekuwapo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi. Kwa njia hii tutasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vilevile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika au kusagika na kuwa sehemu ya udogo. Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake tutafanikiwa. Kumbuka kuwa kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

Maswali :

a. Kipe kisa hiki anwani mwafaka na ueleze sababu (alama 2)
b. Vichafuzi ni nini ? (alama 2)
c. Ongezeko la viwanda limechangiaje uchafuzi wa mazingira ? (alama 2)
d. Tabaka la ozoni huathiriwaje na uchafuzi? (alama 3)
e. Athari zipi zitatokea iwapo mazingira hayatatunzwa ? Fafanua. (alama 4)

f. Kwa nini miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi kuliko sehemu zingine ? ( alama 3)

g. Eleza nui mbili za uchafuzi wa mazingira zilizotajwa katika kifungu hiki. (alama 2)
h. Eleza maana za misamiati ifuatayo kama ilivvotumiwa katika kifungu. (alama 2)

(i) Msambao

(ii) Mazingira

## SEHEMU YA 'C' - MATUMIZI YA LUGHA (Alama 50)

6. a. Tunga sentensi moja ukitumia nomino dhahania **Ala.1**

b. Andika kwa wingi "nyundo hii imevunjika mpini wake" **Ala.1**

c. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali. **Ala.3**

"Mvulana mrefu anavuka barabara

d. Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo **Ala.2**

i. Mtoto mwenyewe alienda shambani

ii. Kazi yetu haihitajiki shuleni

e. Tunga sentensi itakayoonyesha matumizi ya kihusishi cha a-unganifu. **Ala.2**

f. Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. **Ala.2**

Mkulima aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri

g. Badilisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali ya kuamuru **Ala.2**

Baba ingia ndani

h. Eleza maana ya sentensi. **Ala.2**

"Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba na ningalistarehe"

i. Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? **Ala.2**

i) Furaha

ii) Jukwaa

j. Andika katika msemo wa taarifa "Nitakuarifu nikimwona," Elma alisema **Ala.3**

'Mama alishangilia arusi ya mwana'

Anza: Mwana…………………

k. Nyambua kitenzi "ota" kama kinavyotokea katika kirai "Ota Ndoto" ili tofauti tatu zijitokeze. **Ala.3**

l. Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa. **Ala.2**

m. Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno "Chuma" **Ala.2**

n. Kanusha sentensi ifuatayo. **Ala.2**
Mgonjwa huyo alipona na kurejea nyumbani

o. i. Eleza matumizi mawili ya kiambishi - ji- **Ala.1**

ii. Tunga sentensi kuonyesha matumizi hayo **Ala.2**

p. Andika ukubwa wa sentensi ifuatayo. **Ala.2**
"Ndovu wa kiafrika ameharibu kichaka"

q. Ainisha kitenzi kifuatacho. **Ala.2**
"Lililonunuliwa"

r. Toa mifano ya maneno yenye muundo wa silabi ya irabu pekee. **Ala.2**

s. Hizi ni nyakati gani? **Ala.2**

i. Kama saa tisa hivi usiku.

ii. Wakati wa jua kutua.

t. Ziandike sentensi zifuatazo kwa kutumia kirejeshi. Amba- **Ala.2**
i. Ukweli uliobainika umetusaidia

ii. Mayai yaliyokaangwa yameliwa

u. Watu wafuatao hufanya kazi gani? **Ala.3**
i. Mkutubi

ii. Mhazili

iii. Mkadama

v. Unda vitenzi kutokana na nomino hizi. **Ala.2**
i. Hotuba

ii. Tiba

w. Akifisha kifungu hiki. **Ala.3**
Wanyama hawa kiboko ndovu tembo ngiri na ngawa wanyama wa pori wote hupatikana katika mbuga ya maasai mara

## SEHEMU YA 'D' - ISIMU JAMII (Alama 10)

7. a. Nini maana ya isimu jamii. **Ala.2**

b. Eleza dhima ya isimu jamii. **Ala.4**

c. Eleza sifa bainifu za sajili ya mahakamani. **Ala.4**

**P1 – Y2 - KISWAHILI**
**MBINU ZA KUFUNDISHIA**
**MTIHANI WA MWIGO -PP2**
**MACHI, 2018**

**JINA:………………………………………………..**

**NAMBARI YA USAJILI :……………………………**

**UKUMBI: ………………………………………………**

**Maagizo:**

1) Andika Jina lako, Nambari ya usajili na Ukumbi katika nafasi ulizoachiwa.
2) Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi hii.

**SEHEMU YA 'B' – MBINU ZA KUFUNDISHIA (ALAMA.55)**

*Maagizo: Jibu maswali yote*

8. Tayarisha mpangilio wa somo la kusoma ufahamu katika darasa la saba. **Ala.15**

9. Huu ni mfano wa sehemu ya insha ya kudokezwa iliyoandikwa na mwanafunzi wa darasa la sita.

   "Nilikuwa nimemngoja siku jema hiyo aweze kufika so that twende asumbuhi hicho. Alipofika arindai arikuwa na problem mingi sambambu chamba rake irikuwa imefamiwa na wakora. Turiaja kwenda mbolembole kwani, turikuwa tumeshashoka….."

   a. Kwa mfano mmoja mmoja onyesha aina zozote tano za makosa yaliyofanywa na mwanafunzi huyu. **Ala.5**

   b. Ni njia gani utakazotumia kurekebisha kosa moja kuu linalojikariri katika insha hii ili mwanafunzi aweze kuandika insha nzuri. **Ala.5**

5. Wewe ni mwalimu wa darasa la tano na unapanga kufunza kipindi cha redio. Eleza mambo utakayozingatia ili kipindi hiki kiweze kufaulu. **Ala.10**

6. Eleza hatua mbali mbali utakazofuata ukifundisha ngeli ya I – ZI katika darasa la nne. **Ala.10**

7. Thibitisha kwa mifano mwafaka nyenzo mbalimbali utakazotumia kufundishia msamiati wa jikoni katika darasa la tatu. **Ala.10**

**P1 – Y2 - KISWAHILI**
**FASIHI**
**MTIHANI WA MWIGO -PP2**
**MACHI, 2018**

**JINA:…………………………………………………..**

**NAMBARI YA USAJILI :……………………………**

**UKUMBI: ……………………………………………**

**Maagizo:**

1) Andika Jina lako, Nambari ya usajili na Ukumbi katika nafasi ulizoachiwa.
2) Majibu yako yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi hii.

**SEHEMU YA ‘A’ – FASIHI (ALAMA 15)**

***Jibu Maswali Matatu***

**8. USHAIRI**

Chema hakidumu, kingapendekeza,
Sasa ikitimu, Kitakuteleza,
Ukawa na hamu, kukingojeleza
Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza.

Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,
Japo mara fumbi, kinshaniliza,
Na japo siombi, kipate n’ongeza,
Mtu haniambi, pa kujikimbiza.

Chema mara ngapi, kiniondoka,
Mwanangu yu wapi,? Hakukaa mwaka,
Kwa muda mfupi, aliwatilika
Ningefanya lipi, ela kumzika?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,
Alojipa tabu, kwamba anilee,
Na yakwe sababu, nitengenee,
Ilani walihabu, mara amtwee.

Chema wangu poni, kipenzi nyanyanya,
Hadi siku hini, yu moyoni mwangu,

Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,
Ningamtamani, hatarudi kwangu.

Maswali.

a. Hili ni shairi la aina gani na lina bahari zipi? **Ala.4**

---

b. Eleza umbo la beti mbili za mwisho. **Ala.4**

---

c. Maudhui ya shairi hili ni yapi? **Ala.2**

---

d. Toa mfano wa matumizi ya mbinu ya tabdila katika shairi hili. **Ala.2**

---

e. Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa. **Ala.3**

i. Ningamtamani
ii. Hini
iii. Kitatueleza

**<u>SEHEMU B (ALAMA 15)</u>**

**Jibu swali moja katika sehemu hii**

9. J.K.W. Tamthilia

a. Ngwese…… watajaribu kuifunga yangu ndoto. Ehh ndiyo zamu yenyewe ni zamu niliyoisubiri kwa miongo ya miaka……..

i. Ngwese Nalikuwa na Ndoto gani? **Ala.2**

---

ii. Anahofu ndoto itafungwa vipi? **Ala.5**

---

iii. Ametoa sababu gani ya hakika ya ndoto hiyo? **Ala.3**

---

iv. Kama ungekuwa mwanakijiji wa pango ungetoa sababu gani za kutoitimiza ndoto ya ngwese? **Ala.5**

10. Kithaka wa Mbera: Halala.

a. Jadili mbinu tano za uandishi zinazojitokeza katika tamthilia hii. **Ala.5**

**SEHEMU C: RIWAYA (ALAMA 15)**

*Jibu swali mjoa katika sehemu hii.*

11. John Habwe; Maisha Kitendawili.

"Mimi shanidona wazazi wote walikuwa hivi hivi katika muda mmoja. Sasa Kim ndiye huyu, tegemeo langu pekee ashakufa."

a. Eleza Jambo ambalo msemaji wa maneno haya aliweza kuvumbua kutokana na Kifo na Kim? **Ala.1**

b. Taja sababu mbili zilizomfanya msemaji kumpenda kim? **Ala.2**

Msemaji alikusudia uhusiano wake na Kim ungekuwa na manufaa gani katika maisha yake? **Ala.2**

c. Eleza njinsi Kim alivyokumbana na mauti. **Ala.3**

d. Kifo cha Kim kilikuwa chanzo cha matatizo kwa msemaji. Eleza na kufafanua matatizo manne **Ala.3**

e. Kifo cha Kim kilimpa msemaji mafunzo katika maisha yake ya baadaye. Taja matatu kati ya hayo. **Ala.3**

12. LAMIN H. OMAR. Dunia mashaka makuu.

a. Eleza chanzo cha matatizo ya Bw. Mashaka. **Ala.8**

b. Kulingana na mzee mafusho suluhisho la matatizo hayo ni nini? **Ala.7**